**MTANDAO WA WATETEZI WA HAKI ZA BINADAMU**

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU KUKAMATWA BWANA SAMWELI NANGIRA, MKURUGENZI WA SHIRIKLA LA NGONET-LOLIONDO- IMETOLEWA TAREHE 10/4/2016**

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) ambao ni mjumuiko wa asasi zinazotetea haki za binadamu hapa nchini umepata taarifa za kusikitisha na kushtusha kuwa tarehe 08/04/2016 Bwana Samweli Nangiria alikamatwa na kuwekwa mahabusu na polisi huko Loliondo Arusha. Bwana Samuel Nangira ni Mkurugenzi wa Mtandao wa asasi za Kirai Wilayani Ngorongoro (NGONET-Ngorongoro NGOs Network). Taarifa za awali kutoka kwa ofisi ya Kamanda wa Polisi Ngorongoro, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Ngorongoro na Ofisi ya Msajili wa NGOs zinasema kuwa asasi anayoiongoza bwana Samweli haijapata cheti cha ukubalifu kinyume sheria ya Asasi zisizo za Kiserikali (AZISE) ya mwaka 2002 hivyo kupelekea kukamatwa kwake.

Hivi karibuni, baada ya sheria ya AZISE/NGOs ya mwaka 2002 kutungwa na kuanza kutumika kumekuwepo na matakwa katika kipengele cha 11(3) kuzitaka asasi zote za kiraia ambazo hazikusajiliwa chini ya sheria ya NGO bali sheria zingine za usajili wa asasi, kupata cheti cha ukubalifu chini ya Sheria ya NGOs. Ikimbukwe kuwa takriban AZAKI 3000 hapa Tanzania zimesajiliwa kwa sheria mbalimbali ikiwemo sheria ya Makampuni (Companies Act) Sura namba 212; Sheria ya Miunganisho ya Wadhamini(Trustees Incorporation Act) Sura namba 318; Sheria ya Vyama vya Kijamii (The Societies Act)Sura namba 337 na Sheria ya Asasi Zisizokuwa za Kiserikali (AZISE) (NGOs Act) Sheria namba 24 ya mwaka 2002. Sheria zote hizi ni sheria halali nchini na kila shirika la kijami lililosajiliwakwa mujibu wa mojawapo ya sheria hizo, basi linao uhalali wa kisheria kufanya kazi zao kwa mujibu wa sheria husika.

Tunapenda kuwakumbusha kuwa, Sheria ya AZISE ilipotungwa mwaka 2002, kulikuwa na kilio kikubwa toka kwa wadau wakilalamikia mapungufu ya wazi yaliyokuwa katika sheria hiyo. Awali mwaka 2001 wadau walikuwa wameshiriki kikamilifu katika kutunga Sera ya AZISE. Hata hivyo sheria ilipotungwa haikuweza kubeba tunu zilizokuwa kwenye sera ya taifa ya AZISE. Ilionekana wazi kuwa Sheria ya AZISE ilikuwa na masharti yaliyokuwa yanafifisha na kupunguza kabisa mchango wa AZISE kwa taifa. Sheria ya AZISE haikufuta usajili wa asasi yoyote iliyokuwa imesajiliwa awali chini ya sheria nyingine. Kutokana na mapungufu ya wazi katika sheria ya AZISE baadhi ya AZAKI zilizokuwa zimeshasajiliwa kwa masharti ya Sheria nyinginezo, zilisita sana kuridhia baadhi ya vipengele katika sheria ya AZISE ya mwaka 2002,

Ni wazi kuwa sheria ya AZISE ilikuwa na vifungu vyenye masharti kandamizi. Mfano, Sheria hiyo kinakandamiza uhuru wa asasi za kiraia kwa kukiuka misingi ya kikatiba na kitaifa kuhusu haki jinai inayohusina ana mashirika/makampuni. Katika utaratibu wa kawaida shirika linapokuwa limessajiliwa hupewa hadhi ya mtu mbele ya sheria. Hata hivyo kuna adhabu amabazo haiwezekani kulipa shirika - mfano Kifungo, kifo au adhabu ya viboko. Badala yake shirika linapofanya makosa – ahdabu yake ni faini, kufilisiwa au kufutiwa usajili. Pamoja na kuwa wazi kwa taratibu hizo za kisheria –sheria ya AZISE ina hitilafu. Mfano kipengele cha 18 cha sheria hiyo kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2005 kinatamka kuwa asasi iliyosajiliwa kisheria itakuwa na hadhi ya mtu mbele ya sheria na kupewa nguvu ya kushitaki au kushitakiwa mahakamani kama asasi kwa jina lake yenyewe. Wakati huo huo Kifungu cha 36 cha sheria hiyo kinatoa mwanya kwa mamlaka na vyombo vya dola kuwashitaki wafanya kazi wa asasi za kiraia kwa makosa yaliyofanywa na AZISE. Wakati huo huo, Sheria ya AZISE katika kifungu cha 35, inatoa mamlaka ya kukamatwa na kushtakiwa mahakamani kwa kiongozi

wa shirika lolote litakalojiendesha kama AZISE pasipo kupata cheti cha ukubalifu (Certificate of Compliance) kinachotolewa na Msajili wa AZISE Tanzania.

Mtandao umebaini kuwa vifungu vya 35 na 36 ndivyo vilivyoopingwa sana na AZAKI wakati sheria ikitungwa lakini Serikali haikukubali mapendekezo ya AZAKI ili kuvibadilisha. Kwa sasa vifungu hivyo nyimivu kwa haki - ndivyo sasa vinatumika ili kufifisha sauti na michango ya AZAKI kwa taifa; kuikatisha tamaa sekta hii ya hiari; na kubinya uhuru na haki ya kujumuika kama inavyolindwa na Ibara ya 20 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Pamoja na mikataba ya kimataifa na kikanda ambayo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeridhia.

Hadi tunakamilisha tamko hili ni kwamba Bwana Samweli yupo maabusu siku ya tatu leo bila dhamana na anategemewa kufikishwa Mahakamani siku ya Jumatatu tarehe 11/04/2016. Kutokana na hali hiyo Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) tunapenda kusisitiza yafuatayo; :-

i. Tunatambua kazi kubwa inayoikabili ofisi ya Msajili wa AZISE katika kusimamia sheria, sera, kanuni na taratibu na tunaunga mkono juhudi zote zitakazofanywa kwa ajili ya kuhakikisha kuwa haki ya uhuru wa kujumuika inaheshimiwa nchini Tanzania.
ii. Tunaunga mkono na kupongeza juhudi zote zinazofanywa kwa nia nzuri na ofisi ya Msajili wa AZISE na ofisi za wasajili wengine za kutaka kuona sector ya AZAKI iliyobora, makini, yenye tija kwa umma na zaidi yenye kufuata sheria zinazotoa mamlaka kwa AZAKI.
iii. Tunatambua kuwa kuna mikakati mingi inafanyika kuhusu usajili na uratibu wa AZAKI nchini bila ushiriki wa AZAKI. Tunawasihi wahusika waone umuhimu wa kushirikisha AZAKI katika kila hatua ya mazungumzo ili kuepuka mapingamizi baadaye katika chochote watakachoamua.
iv. Tunataka Bwana Samweli aachiwe na kufutiwa mashitaka na badala yake Asasi ndiyo ifunguliwe mashitaka kama itakuwa imekwenda kinyume na sheria iliyoridhia usajili wake na iliyotoa na mamlaka ya kufanya kazi zake wilayani Ngorongoro .
v. Tunataka Sheria ya AZISE ya mwaka 2002 ifanyiwe marekebisho hasa vipengele vyote kandamizi kama vile kipengele cha 18, 35, 36 na vinginevyo.
vi. Tunawashauri wana AZAKI wote kujitahidi kufuata taratibu zote za kisheria hasa kuzingatia sheria zilizowapa mamlaka ya kufanya kazi zao baada ya kusajiliwa.
vii. Tunawaomba wasajili wote waungane na wana AZAKI nchini na kukaa pamoja kujadili changamoto za kisheria na za kiutendaji zinazoikumba sector ya AZAKI badala ya kuzifungia AZAKI . Tunaamini suala hili likiendeshwa kwa nia njema na bila kuviziana ni rahisi kupata suluhisho la kudumu tena kwa muda mfupi na bila gharama kubwa.
viii. Tunashauri Msajili wa NGOs aitishe mkutano na AZISE kwa kushirikiana wasajili wengine wa AZAKI pamoja na wawakilishi/mitandao ya AZAKI zote nchini zilizosajiliwa chini ya sheria zingine ili kujadili na kupata ufumbuzi wa suala la kisheria lenye utata mwingi kuhusiana na cheti cha ukubalifu (Compliance Certificate).
ix. Tunashauri viongozi wetu wa serikali waone tasnia ya AZAKI kama kiungo muhimu kwa ustawi wa jamii hasa katika masuala ya ajira, uchumi, ustawi na huduma za jamii, maendeleo, haki za binadamu na ustawi wa democrasia nchini. Hivyo tasnia hii ya AZAKI ipewe heshima , ulinzi, utambuzi na ushirikiano badala ya kubezwa na kutengwa hata katika masuala yahusuyo uratibu na usajili wao.

**Imetolewa leo tarehe 10/4/2016 na;**

**Onesmo Olengurumwa, Mratibu wa Kitaifa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania**